






Kisa cha Sungura Mjanja







Jioni ng'ombe, mbuzi, kondoo walirudi kutoka malishoni. Mfugaji aliwaongoza wote kuingia kwenye banda lao.

Sungura mjanja alikuwa macho kwenye banda akiwaza, “Ninataka kwenda nje.” Sungura wengine walisinzia.



Mara mlango wa banda
ulifunguliwa.
Mfugaji alileta chakula.




Chakula kile kilinukia vizuri. Sungura wote waliamka. Wote walimsogelea mfugaji.





Sungura mjanja alimtazama mfugaji. “Ahaa! Najua nitatoka vipi. Lazima kesho nitoke.”



Sungura walikula na kushiba. Baada ya muda usingizi uliwapitia.



Asubuhi ilipofika, mfugaji aliwaletea sungura chakula chao. Sungura mjanja alisema, “Leo ni lazima nitoke bandani.”



Sungura mjanja aliingia kwenye kapu la mfugaji bila kuonekana.






Sungura njanja alitoka ndani ya kapu akiwa na furaha. Aliimba huku akitembea kwa madoido. Mara mbele yake akatokea mbwa. Mbwa alipomuona sungura mjanja alibweka.



Mbwa alianza kumkimbiza
sungura mjanja.




Mbwa alimkimbiza lakini
sungura mjanja alikimbia zaidi
ya mbwa.





Sungura mjanja alimtoroka mbwa, aliingia msituni. Aliona majani mazuri. Alikula majani mpaka akashiba. Usingizi ulimpitia.






Mara, sungura mjanja aliamshwa na mngurumo wa simba. Simba aliunguruma kwa sauti ya kutisha.



Simba yule alikuwa akitafuta chakula msituni. Simba alianza kumkimbiza sungura mjanja. Sungura mjanja alianza kukimbia.



Sungura mjanja alikimbia kwa nguvu zake zote, huku akiwaza, “Lo! Nitapona kweli leo?” Alikimbia usiku kucha. Hakujua anakoelekea.



Kulipokucha, hakuamini. Alijikuta karibu na nyumba ya mfugaji. Jasho lilimtoka huku akihema sana.



Sungura mjanja alichoka na alikuwa na njaa kali. Mlango wa banda ulikuwa wazi. Mfugaji alikuwa akiwapa sungura wengine chakula.



Sungura mjanja alinyata na kuingia ndani.



Kwa njaa aliyokuwa nayo, alikula sana.
Sungura mjanja aligundua, dunia ya nje ina
raha na taabu zake.



Toka siku ile sungura mjanja alikuwa mpole
na mshauri mzuri kwa wenzake.

